**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA AFYA

**MKOA WA IRINGA**
Simu Na: 026 - 2702264
Fax. 026 – 2702264
Barua pepe iringarrh@afya.go.tz
**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb.Na** IRRH/L.10/1/Vol.II/70

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,
Mtaa wa Kinondoni,
S. L. P. 260
**IRINGA**

26 Januari, 2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUJITOLEA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa IRINGA anatangaza nafasi 43 za ajira ya kujitolea kwa kada mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. **Daktari Daraja la II(Medical Doctors II) – Nafasi 11**

   Sifa wenye Shahada ya Udaktari kutoka Vyuo Vikuu/ Vyuo vinavyotambulika na serikali waliomaliza mafunzo ya kazi "Intership" ya muda usiopungua miezi Kumi na miwili na kupata usajili katika Baraza la Madaktari Tanganyika(Medical Council of Tanganyika)

2. **Mfamasia Daraja la II(Pharmacists II) – Nafasi 02**

   Sifa wenye shahada ya Famasi kutoka chuo kinachotambulika na Serikali aliyehitimu mafunzo ya vitendo kazini(Internship) ya mwaka mmoja ambao wamesajiliwa na Baraza la Famasi.

3. **Afisa Muuguzi Msaidizi II – Nafasi 20**

   Sifa wenye Stashahada(Diploma) ya Uuguzi ya muda usiopungua miaka miwili(2) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania

   - **Mwenye sifa ya ziada ikiwemo mafunzo ya cheti katika fani ya usingizi (Anaesthetist) atafikiriwa kwanza**

4. **Mteknolojia Dawa II(Pharmacetical Technologist) – Nafasi 05**

   Sifa wenye stashahada katika fani ya Uteknolojia wa dawa ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza la Famasia.

5. **Mtoa Tiba kwa Vitendo II (Occupational Therapist II) – Nafasi 01**

   Sifa awe muhitimu wa kidato cha nne/sita mwenye stashahada ya miaka mitatu katika fani ya mtoa tiba kwa vitendo katika Chuo kinachotambulika na Serikali.

6. Afisa Ustawi wa Jamii II – Nafasi 02

Sifa awe na Shahada ya B A (Social work/Socialogy) au Stashahada ya juu ya Ustawi wa Jamii(Advanced Diploma in Social work) kutoka Chuo cha Elimu ya Juuu kinachotambuliwa na serikali

7. **Afisa Hesabu II (Accounts Officer) – Nafasi 02**

Sifa awe na shahada ya Sanaa/Biashara aliyejiimarisha kwenye fani ya Uhasibu au Stashahada ya Juu ya Uhasibu katika Taasisi yoyote inayotambuliwa na serikali

**Mambo Muhimu ya Kuzingatia kwa Mwombaji**

a) Mwombaji awe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
b) Awe na cheti cha ufaulu cha kidato cha nne(IV) au sita(VI)
c) Awe na cheti cha ufaulu cha taaluma husika
d) Awe na cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)
e) Ambatanishe wasifu wake (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na wadhamini (Refeers) watatu wa kuaminika
f) Awe na picha mbili (2) "Passport size" alizopiga hivi karibuni
g) Awe na nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)
h) Waombaji waliosomo nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinisha na mamlaka husika (NACTE na NECTA)
i) Barua za uthibitisho/matokeo ya mtihani(Testimons/Provisional/Statements of result) hazitapokelewa
j) Uwasilishaji na Taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

**Malipo ya Mishahara wa mwezi yatalipwa nusu mshahara kwa kuzingatia ngazi ya mishahara kwa kila kada husika (TGHS E, D, B na TGS D) na mikataba itakuwa kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu (3).**

Barua zote za maombi haya zitumwe/ziwasilishwe kwa anuani ya :-

**Mganga Mfawidhi,**
**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,**
**S L P. 260,**
**IRINGA**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **11 Februari, 2022** saa **9:30 Alasiri**, wote wenye sifa wanakaribishwa

Imetolewa na

Dkt Alfred M Laison
Mganga Mfawidhi
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
**IRINGA**